TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TUME YA UTUMISHI WA UMMA JANUARI 2004 HADI JUNI 2005

1.0 UTANGULIZI:

Taarifa hii imeandaliwa kwa mujibu wa Kifungu Na. 16(1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002 kinachoitaka Tume kutoa taarifa kwa Mheshimiwa Rais kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Tume na taarifa za matumizi ya Tume kwa kipindi cha mwaka uliopita, kifungu hicho pia 16(2) kinamtaka Waziri Mwenye Dhamana na Utumishi wa Umma baada ya Mheshimiwa Rais kukabidhiwa Taarifa hii awasilishe katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Taarifa hii pia itaonyesha mambo yafuatayo:-

- Hali ya Utumishi wa Umma itakayojumuisha idadi ya watumishi wa Umma, viwango vya elimu na Mfumo wa Uboreshaji Utendaji kazi Serikalini.
- Utekelezaji wa masuala ya ajira na nidhamu katika utumishi wa umma kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002, Kanuni na Taratibu za Uendeshaji katika Utumishi wa Umma za mwaka 2003.
- Hatua zilizochukuliwa na Tume katika kurekebisha kasoro zilizojitokeza katika kuboresha Utumishi wa Umma.
- Changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Sheria Na. 8 ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2002.
- Matarajio ya Tume kwa kipindi kijacho.

2.0 MUUNDO NA MAJUKUMU YA TUME

Muundo na majukumu ya Utumishi wa Umma kwa mujibu wa Sheria Na.8 ya mwaka 2005 ni kama ifuatavyo:-

2.1 MUUNDO WA TUME

Kwa mujibu wa kifungu Na.9(1), cha Sheria Na.8 ya Utumishi wa Umma 2002 kikisomwa pamoja na Kifungu 14(1)Tume inaundwa na Mwenyekiti na Wajumbe wasiozidi sita (6) na Katibu wa Tume ambao wote huteuliwa na Rais.

Kwa kipindi hiki Tume iliongozwa na viongozi wafuatao:-

1.	Jaji Mstaafu Lameck M. S. Mfalila	-	Mwenyekiti
2.	Bw. Leonard K. Msaki	-	Mjumbe
3.	Bibi Monica G. Mbapila	-	Mjumbe
4.	Balozi Norman A. Kiondo	-	Mjumbe
5.	Bibi Nderikyo E. Ligate	-	Mjumbe
6.	Bw. Ashour A. Abbas	-	Mjumbe
7.	Bw. Kenya A. Hassan	-	Mjumbe
8.	Bibi Thecla W. Shangali	-	Katibu

2.1.1 Idara za Tume

Kwa mujibu wa Sheria Na.8 ya mwaka 2002, kifungu Na.15(1) Tume imegawanyika katika Idara tano (5) ambazo ni:-

- Idara ya Utumishi Serikalini
- Idara ya Utumishi wa Walimu.
- Idara ya Utumishi wa Serikali za Mitaa.
- Idara ya Utumishi wa Uhamiaji, Zimamoto na Uokoaji.
- Idara ya Utumishi wa Afya.

Idara hizi zinaongozwa na Manaibu Katibu wa Tume.

Aidha, Tume ina Idara ya Utawala na Utumishi ambayo inajumuisha pia vitengo vya Uhasibu, Mifumo ya Habari, Ukaguzi wa Ndani, Sheria, Maktaba, Kompyuta na Takwimu.

Tazama Kiambatisho A.

2.2 MAJUKUMU YA TUME

Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Umma yaliyoainishwa kwenye kifungu Na. 10(1) cha Sheria Na.8 ya mwaka 2002 ni:-

- Kumshauri Rais kupitia ofisi ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma katika kutekeleza majukumu yake aliyopewa kikatiba chini ya Ibara ya 36 kuhusu ujazaji wa nafasi zilizo wazi katika Utumishi wa Umma kama Rais atakavyohitaji.
- Kumshauri Rais kuhusu masuala ya Utumishi kama atakavyohitaji.
- Kutoa miongozo, kufuatilia na kuhoji taratibu zilizotumika na mamlaka za ajira katika kutekeleza kazi za ajira na uthibitishwaji kazini, ili kuhakikisha kuwa misingi ya uwazi na sifa imezingatiwa kikamilifu
- Kuwezesha uteuzi na ajira za nafasi mbalimbali katika Utumishi wa Umma
- Kuwezesha, kufuatilia na kutathimini utendaji kazi wa watumishi wa Umma wa ngazi mbalimbali ili uwe na ufanisi na unaowajali wateja na wenye kuzingatia matokeo (result oriented).
- Kusimamia na kufuatilia uzingatiaji wa kanuni na maadili katika utendaji kazi wa viongozi wa Utumishi wa Umma hususan katika maeneo ya mafunzo, ajira, upandishwaji vyeo na mashtaka ya nidhamu ya watumishi.
- Kupokea na kushughulikia rufaa kutoka kwa watumishi na Mamlaka mbali mbali za Nidhamu katika Utumishi wa Umma.

- Kuwaita na kupata maelezo kutoka kwa viongozi na watendaji pale inapokuwa na ushahidi au malalamiko yanayoonesha usimamizi au utendaji usioridhisha kinyume cha shabaha na madhumuni ya Utumishi wa Umma.
- Kuhakikisha kuwa taratibu za uendeshaji katika Utumishi wa Umma za makundi mbalimbali ya Utumishi zinatungwa na kutekelezwa ipasavyo.
- Kuwachukulia hatua kupitia kwa mamlaka zao za nidhamu viongozi na watendaji watakaoshindwa kuwashughulikia watumishi walio chini yao kwa mujibu wa Kanuni na taratibu zinazosimamia utendaji kazi katika Utumishi wa Umma.
- Kuzishauri na kuzisaidia mamlaka mbalimbali za ajira katika masuala mbalimbali ya Utumishi wa Umma kadri itakavyoombwa au itakavyoona inafaa.

3.0 HALI YA UTUMISHI WA UMMA

Katika kipindi hiki Tume ilianzisha zoezi la kukusanya kumbukumbu za watumishi wa umma ili kujua idadi yake, jinsia na viwango vya elimu kwa kila kada. Zoezi hili bado linaendelea. Hata hivyo takwimu zilizopatikana kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma zinaonyesha kuwa kuna jumla ya watumishi wa umma 304,054 kati yao wanaume 147,665 wanawake 98,828 na wasiofahamika jinsia ni 57,561 ambao ni sawa na asilimia 18.9 ya watumishi wote wa Umma. Watumishi hawa ni wapya na bado hawajaingizwa kwenye mfumo wa Kompyuta ya Watumishi wa Umma.



Chanzo : Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, 2005

3.1 Viwango vya Elimu.

Viwango vya Elimu vya Watumishi wote 304,054 vimegawanyika kama ifuatavyo:-

Jedwali 1 : Viwango vya Elimu vya Watumishi wa Umma kwa Jinsia

		Jinsia			
Na.	Kiwango cha Elimu	Isiyojulikana	Ke	Me	Jumla
*1	Viwango vya Elimu Haijulikani	56,769	3,269	4,941	64,979
2	Daktari wa Falsafa	2	16	138	156
3	Stashahada ya juu	12	792	2,632	3,436
4	Shahada	10	772	2,736	3,518
5	Uzamili	4	429	1,448	1,881
6	Stashahada ya uzamili	4	149	598	751
7	Stashahada	59	5,567	12,947	18,573
8	Kidato cha V - VI	52	966	3,751	4,769
9	Kidato cha I - IV	490	38,866	55,999	95,355
10	Elimu ya msingi Darasa la V-VIII	157	47,337	59,510	107,004
11	Darasa la IV	2	665	2,965	3,632
	JUMLA	**57,561**	**98,828**	**147,665**	**304,054**

Chanzo: Ofisi ya Rais Menejiment ya Utumishi wa Umma, 2005

* Watumishi hawa ni wapya na bado hawajaingizwa kwenye mfumo wa Kompyuta.



Chanzo : Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, 2005

Jedwali la hapo juu linaonyesha kwamba karibu asilimia 36 ya watumishi waliomo katika Utumishi wa Umma ni wale wenye elimu chini ya Kidato cha Nne. Na kwa mujibu wa Sera ya Ajira na Menejimenti ya Utumishi wa Umma ya mwaka 1998 na Waraka wa utumishi wa umma Na.1 (Establishment) mwaka 2004, sifa ya chini ya elimu ya kuajiriwa katika Utumishi wa Umma ni Kidato cha Nne. Aidha kati ya watumishi 304,054 wa umma, watumishi 110,636 hawajafikia Kidato cha Nne na wamepewa muda wa kujiendeleza hadi kufika kiwango hicho ifikapo

mwaka 2007. Mbali na hawa kuna jumla ya watumishi 64,979 sawa na asilimia 21 ambao viwango vyao vya elimu havijulikani.

3.2 Mfumo wa Uboreshaji Utendaji Kazi Serikalini.

Madhumuni ya kuanzisha kwa mfumo huu ni pamoja na kujenga uwezo wa watumishi na asasi za umma ziweze kuboresha utoaji huduma, tija, uwajibikaji, usimamizi wa kazi na uendelezaji wa Rasilimali watu katika Utumishi wa Umma. Mfumo huu unajumuisha hatua zifuatazo:-

- Mpango mkakati (Strategic plan)
- Mpango wa muda wa kati wa matumizi na bajeti (Medium Term Expenditure Framework)
- Ratiba ya kazi za mwaka (Action plan)
- Mkataba wa huduma kwa mteja (Clients Service Charter)
- Mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya utendaji (Monitoring and Evaluation)
- Mfumo wa wazi wa kupima utendaji kazi wa mtumishi (OPRAS).

Kwa upande wa uendeshaji na usimamizi katika Utumishi wa Umma mfumo huu unazingatia utendaji kazi unaojali matokeo. Aidha, umeweka utaratibu thabiti wa uwajibikaji kwa ngazi ya Taasisi na kwa ngazi ya Mtumishi binafsi.

Katika kipindi hiki Tume ya Utumishi wa Umma haijaweza kufanya ukaguzi katika eneo hili ambalo ni moja ya kazi za Tume kwa mujibu Sheria Na.8 ya mwaka 2002, kifungu cha 10 (1)(g). Hata hivyo kwa mujibu wa taarifa za Ofisi ya Rais

Menejimenti ya Utumishi wa Umma mfumo huu umeanzishwa Serikalini na kutekelezwa kama ifuatavyo:-

- Umekamilika katika Wizara 25, Idara zinazojitegemea 11, na Wakala za Serikali 20 na
- Umeanzishwa kwenye Mikoa yote 21 ya Tanzania Bara, bado upo kwenye hatua za ukamilishwaji, ambapo Mikoa tisa ya Mwanza, Kagera, Mara, Shinyanga, Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Tanga na Mbeya imefundishwa OPRAS na Mikoa kumi na mbili iliyobaki bado haijafundishwa.

Jedwali 2 : Hali ya Utekelezaji wa Mfumo wa Uboreshaji Utendaji Kazi Serikalini

NA.	WIZARA	HALI YA UTEKELEZAJI (STATUS)											MAFANIKIO ASILIMIA
		SDS	SA	SP	TOP RAS	OP	AP	IPA	CSC		PIF		
									D	I	T	D	
1	Menejimenti ya Utumishi wa Umma	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	100
2	Wizara ya Maji na Mifugo	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	100
3	Wizara ya Kilimo na Chakula	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	100
4	Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	100
5	Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango na Ubinafsishaji	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	100
6	Wizara ya Fedha	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	100
7	Wizara ya Afya	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	100
8	Wizara ya Ushirika na Masomo	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	100
9	Wizara ya Elimu na Utamaduni	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	100
10	Wizara ya Sheria na Katiba	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	100
11	Wizara ya Maliasili na Utalii	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	100
12	Ofisi ya Makamu wa Rais	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	100
13	Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	100
14	Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	100
15	Ofisi ya Rais, Ikulu	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	100
16	Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	100
17	Wizara ya Mambo ya Ndani	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	100
18	Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	100
19	Wizara ya Madini na Nishati	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	100
20	Wizara ya Ujenzi	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	100
21	Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	100
22	Wizara ya Viwanda na Biashara	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	100
23	Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	100
24	Ofisi ya Waziri Mkuu	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	100
25	Wizara ya Ardhi, na Maendeleo ya Makazi	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	100
	IDARA ZINAZOJITEGEMEA												
1	Idara ya Mahakama ya Rufaa	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	√	100
2	Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali	√	√	√	√	√	√	√	√		√		90
3	Tume ya Kurekebisha Sheria	√	√	√	√	√	√	√	√		√	√	100
4	Mahakama ya Biashara	√	√	√	√	√	√	√	√		√		90
7	Ofisi ya Bunge	√	√	√	√	√	√	√			√		90

NA.	WIZARA	HALI YA UTEKELEZAJI (STATUS)											MAFANIKIO ASILIMIA
		SDS	SA	SP	TOP RAS	OP	AP	IPA	CSC		PIF		
									D	I	T	D	
8	Tume ya Uchaguzi	√	√	√	√	√	√	√			√		90
9	Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi	√	√	√	√	√	√	√			√		90
10	Tume ya Kudhibiti UKIMWI	√	√	√	√	√	√	√			√		90
11	Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa												
12	Tume ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya												
13	Tume ya Haki za Binadamu	√	√	√	√	√	√	√	√		√		90
14	Sekretarieti za Mikoa 21			√	√	√	√	√	√		√		72
	WAKALA WA SERIKALI												
1	Wakala wa Uchimbaji Visima na Mabwawa	√	√	√	√	√	√	√	√		√	√	100
2	Kituo cha Tanzania cha Mafunzo ya Maendeleo Duniani			√	√	√	√	√			√		54
3	Chuo cha Utumishi wa Umma			√	√	√	√	√			√		54
4	Mkemia Mkuu wa Serikali			√	√	√	√	√			√		54

Chanzo : Hotuba ya Bajeti ya Mawaziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa 2005/06

4.0 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TUME

Katika kipindi hiki, Tume imetekeleza na kukamilisha kazi kama ifuatavyo:-

4.1 Kukamilisha kazi zilizoachwa na Tume zilizovunjwa.

Tume ilikamilisha kazi zilizokuwa mikononi mwa Tume zilizovunjwa pamoja na kushughulikia kazi zilizokuwa kwa Waajiri ambazo zilitakiwa zifanywe kwa kutumia Tume zilizovunjwa za kupandisha vyeo na kushughulikia masuala ya Nidhamu na Rufaa. Kazi hizo zilifanywa kwa mujibu wa Agizo la Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma la tarehe 12/3/2004 kama ifuatavyo:-.

4.1.1 Kupandisha Vyeo na Kuthibitisha Watumishi

Tume iliwapandisha vyeo watumishi 44,803, kuwabadilisha vyeo watumishi 1,617 na kuwathibitisha kazini watumishi 288 kama ifuatavyo:-

Jedwali la 3 : Watumishi Waliopandishwa na Kuthibitishwa vyeo.

Tume iliyovunjwa	Kupandishwa vyeo	Kuthibitishwa kazini	Kubadilishiwa cheo

Utumishi wa Walimu	30,434	-	1,335
Utumishi Serikalini	10,421	288	282
Utumishi wa Serikali za Mitaa	3,948	-	-
Jumla	44,803	288	1,617

Chanzo : Tume ya Utumishi wa Umma, 2005



Chanzo : Tume ya Utumishi wa Umma, 2005

Chati hii inaonyesha kwamba katika kushughulikia kazi zilizokuwa kwenye Tume zilizovunjwa, Tume ya Utumishi wa Walimu ilikuwa na kazi nyingi ambazo hazikukamilishwa ikifuatiwa na Tume ya Utumishi Serikalini na Tume ya Utumishi Serikali za Mitaa.Tume ya Utumishi Serikalini ilishughulikia pia Utumishi wa Afya na Uhamiaji ambao Utumishi huo uko chini ya Idara za Tume husika.

4.1.2 Masuala ya Nidhamu na Rufaa:

Tume imejadili na kuyatolea maamuzi mashauri ya nidhamu 415 na rufaa 28 kama ifuatavyo:-

Jedwali la 4: Mashauri ya Nidhamu na Rufaa

Tume iliyovunjwa	Mashauri		Maamuzi
	Nidhamu	Rufaa	

Utumishi wa Walimu	403	-	351 – Walifikuzwa kazi. 41 – Walirudishwa kazini. 8 – Uchunguzi unafanyika. 3 – Yaundiwe jopo la madaktari.
Utumishi wa Serikali za Mitaa	12	-	7 – Walirudishwa kazini. 4 – Walifukuzwa kazi. 1 – Mapendekezo yalipelekwa TAMISEMI.
Utumishi Serikalini	-	28	12 – Zilikubaliwa 16 – Zilikataliwa
JUMLA	**415**	**28**	**443**

Chanzo : Tume ya Utumishi wa Umma, 2005

4.2 Utekelezaji wa majukumu kwa mujibu wa Sheria Na 8 ya 2002:

Tume imetekeleza majukumu yake iliyopewa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002 kifungu cha 10(1) kama ifuatavyo:-

4.2.1 Kuziwezesha Mamlaka za Ajira na Nidhamu:

Tume imeziwezesha mamlaka mbalimbali za Ajira na Nidhamu kwa kuzipatia mafunzo katika masuala ya usimamizi, uendeshaji na udhibiti wa ajira na nidhamu katika Utumishi wa Umma. Uwezeshaji huo ulifanyika kama ifuatavyo:-

(a) Kushiriki kwenye Semina na Mikutano ya wadau:

Tume ilishiriki na kutoa mafunzo katika mikutano ya wadau kama ifuatavyo:-

Jedwali la 5 : Mikutano ya Wadau Tume iliyoshiriki

Tarehe	Mwandaaji	Mkutano	Mahali
24-25/11/2004	Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma	Wakurugenzi wa Utawala na Utumishi na Maafisa Tawala Wafawidhi wa Mikoa	Arusha
1-4/12/2004	Katibu Mkuu Kiongozi Ikulu	Makatibu Wakuu na Makatibu Tawala wa	Mwanza

		Mikoa.	
16 – 17/12/04	ALAT	Jumuiya ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (ALAT)	Tabora
5 – 6/01/05	Mkurugenzi wa Uhamiaji	Maafisa Uhamiaji wa Mikoa na Vituo vya mipakani	Tanga
10 – 12/02/05	Katibu Mkuu TAMISEMI	Baraza la Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa.	Morogoro

Chanzo : Tume ye Utumushi wa Umma, 2005

(b) Vikao vya Kazi:

Tume iliandaa vikao vya kazi kwa lengo la kujadiliana na kuelekezana namna ya kutekeleza kwa ufanisi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za uendeshaji wa Utumishi wa umma. Vikao hivyo ni:-

Jedwali 6 : Vikao vya Kazi vilivyoandaliwa na Tume

Na	Tarehe	Kikao cha Kazi	Madhumuni	Mahali	Idadi ya washiriki
1.	5/10/2004	Wadau wa Zimamoto na Uokoaji	Kujadili hali ya Utumishi wa Zimamoto na Uokoaji nchini ili kuboresha utendaji kazi	DSM	42
2.	22-26/11/04	Makatibu wa mikoa na Wilaya wa TSD.	Mapitio ya Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002	Arusha	151
3.	1-5/3/2005	Wakurugenzi wa Halmashauri	Mapitio ya Sheria ya utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002.	Arusha	97
4.	7-11/3/05	Maafisa Utumishi wa Halmashauri	Mapitio ya Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002	Arusha	94
5.	14-16/3/05	Wenyeviti wa Bodi za ajira katika Halmashauri	Utekelezaji wa majukumu ya Bodi za Ajira	Arusha	93

6.	21-23/3/05	Wasaidizi Wakuu wa Wakurugenzi wa Utawala na Utumishi	Kutoa mafunzo na kubadilishana uzoefu kuhusu uboreshaji wa Utumishi wa Umma na utekelezaji wa Sheria Na.8 ya mwaka 2002 na Kanuni na Taratibu za mwaka 2003 na nyaraka mbalimbali na miongozo ya Tume.	Morogoro	59
7.	22-23/4/05	Wenyeviti wa Kamati za Ajira za Mikoa na Wilaya TSD	Mapitio ya Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002.	Morogoro	130
8.	25 –9/4/05	Wadau wa Walimu wizara ya Elimu na Utamaduni, Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, Wizara ya maendeleoa ya jamii Jinsia na Watoto, CWT na Watendaji.	Kuelekeza Sheria Na.8 ya Utumishi wa Umma 2002 na kanuni zake mwaka 2003	Morogoro	36

9.	26-27/5/05	Maafisa na Makamanda Zimamoto	Kujadili kwa kina juu ya utumishi wa Zimamoto na Uokoaji nchini na kupanga mikakati ya pamoja ya kuimarisha utumishi wa Zimamoto na Uokoaji nchini kwa mujibu wa sheria Na. 8 ya mwaka 2002.	Moshi	64
10.	30-31/5/05	Maafisa Uhamiaji wa Mikoa na vituo vya mpakani	Kujadili kwa kina juu ya Utumishi wa Uhamiaji nchini na kupanga mikakati ya pamoja ya kuimarisha Utumishi wa Uhamiaji nchini kwa mujibu wa Sheria Na.8 ya mwaka 2002.	Moshi	58
11.	6–11/6/05	Wakuu wa vyuo vya afya na wawakilishi wanaoshughulikia masuala ya utawala katika hospitali za rufaa	Kuwaelemisha wakuu wa vyuo kuhusu mabadiliko ya utumishi ili nao wawaelimishe wanafunzi wa kada mbalimbali za Afya.	Morogoro	60

12.	27-29/6/05	Makatibu Tawala Wasaidizi Mikoa (Staff Service Cluster) Maafisa Utumishi Mikoa, Makatibu wa TSD Mikoa	Kujadili na kuelemishana juu ya sheria ya Utumishi wa umma, utekelezaji wa majukumu mapya ya Tume ya Utumishi wa Umma, Mamlaka za Ajira na Nidhamu na kupanga mikakati wa pamoja wa kuimarisha Utumishi wa Umma.	Moshi	78

Chanzo : Tume ya Utumishi wa Umma, 2005

(c) Kuitangaza Tume:

Wadau mbalimbali waTume ya Utumishi wa Umma wameelimishwa kuhusu muundo, majukumu ya Tume na taratibu mpya katika masuala ya usimamizi, uendeshaji na udhibiti wa ajira, upandishwaji vyeo na nidhamu katika utumishi wa umma kwa njia zifuatazo:

- **Ziara za Tume**

Mwenyekiti na Makamishna wamefanya ziara katika Mikoa ya Dodoma, Tanga, Kigoma, Mtwara, Mara, Ruvuma, Singida, Kagera, Arusha, Kilimanjaro, Pwani Mbeya, Tabora, Mwanza, Lindi, Rukwa, Morogoro na pia imetembelea Tanzania Visiwani na kukutana na watumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Mambo yaliyojitokeza kwenye ziara hizi yataelezwa kwa undani kwenye 6.0

- **Kutoa Vipeperushi, Majarida, T-shirt na Kofia**

  Tume imechapisha na kusambaza kwa wadau vipeperushi 20,000, majarida 10,000, T-shirt 4,020 na Kofia 2,000.

- **Kushiriki kwenye Maonyesho ya Kitaifa**

  Tume imeshiriki kwenye maonyesho ya maadhimisho ya wakulima Nanenane, 2004 Morogoro, na sikukuu ya siku ya sherehe ya Serikali za Mitaa iliyofanyika jijini Dar es Salaam tarehe 27//6 – 1/7/2005.

- **Kushiriki kuendesha vipindi vya Redio.**

  Tume imetangaza vipindi 52 vya "Ijue TSD" ambavyo hutoka kila siku ya Ijumaa saa 12.45 hadi saa 1.00 usiku.

4.2.2 Kuwezesha Ajira na Uteuzi katika Utumishi wa Umma:

Tume katika kipindi hiki imeiwezesha ajira na uteuzi katika Utumishi wa Umma kama ifuatavyo:-

(a) Kufanya Usaili:

Tume imefanya usaili na kuwasilisha matokeo ya usaili kwa Mamlaka za Ajira husika kwa uteuzi kama ifuatavyo:-

Jedwali la 7 : Usaili uliofanywa na Tume kwa niaba ya Mamlaka za Ajira

Tarehe	Mamlaka ya Ajira	Nafasi Wazi	Idadi
1-4/3/2004	Katibu wa Tume Haki za Binadamu na Utawala Bora.	– Mkurugenzi wa Mafunzo na Elimu ya Umma – Mkurugenzi wa Utafiti na Mweka Kumbukumbu – Mkurugenzi wa Utawala wa Sheria. – Mkurugenzi wa Masuala ya Sheria. – Mkurugenzi wa Hazi za Binadamu. – Mkaguzi wa Ndani Mkuu. - Mchambuzi wa Kompyuta Mwandamizi	1 1 1 1 1 1 1
27-28/9/04	Morogoro Singida Manyara Mwanza Shinyanga Tabora Mbeya Kigoma Kilimanjaro	Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa	5 5 5 5 4 5 5 1 5
26/2/2005	Makatibu Tawala wa Mikoa - Mara - Rukwa - Iringa	Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa " "	 5 5 5
27-29/6/05	Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara	– Mkurugenzi wa Sera, Mipango na Ubinafsishaji – Mkurugenzi wa Biashara – Afisa Biashara Mkuu I - Afisa Biashara Mkuu II	1 1 1 2
	Jumla		**67**

Chanzo : Tume ya Utumishi wa Umma, 2005

(b) Kushiriki katika Kamati Maalum za Ajira na Bodi za Ajira

Tume imeshiriki katika Kamati Maalum za Ajira na Bodi za Ajira kwenye zoezi la usaili kama ifuatavyo:-

Jedwali la 8 : Ushiriki wa Tume kwenye Kamati Maalum za Ajira na Bodi za Ajira

KAMATI MAALUM ZA AJIRA				BODI ZA AJIRA/ HALMASHURI
WIZARA	**IDARA ZINAJITEGEMEA**	**WAKALA WA SERIKALI/TAASISI ZA UMMA**	**SEKRETARIETI ZA MIKOA**	
1. Fedha	Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi	Mamlaka ya Hali ya Hewa	Tanga	Kondoa
2. Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo	Tume ya Utumishi wa Umma	Kituo cha Uwekezaji	Mtwara	Kibaha
3. Viwanda na Biashara	Tume ya Haki ya Binadamu NA Utawala Bora	Insurance Supervisory Dept.	Mwanza	Rombo
4. TAMISEMI	Tume ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya	Kituo cha zama za kilimo na ufundi Vijijini (carmatec)	Singida	Arusha
5. Ushirika na Masoko	Tume ya Kudhibiti	Mbegu za Kilimo	Mara	Ngorongoro

	Ukimwi			
6. Maji na Maendeleo ya Mifugo	Idara ya Mahakama	Mamlaka za Ndege Tanzania	Iringa	Serengeti
7. Nishati na Madini	Tume ya Kurekebisha Sheria	Ndege za Serikali	Arusha	Handeni
8. Ofisi ya Makamu wa Rais	Tume ya Taifa ya Uchaguzi	Chuo cha Hoteli ya Utalii	Dodoma	Same
9. Menejimenti ya Utumishi wa Umma	Uhamiaji	Utafiti wa nyumba (National Housing Building and Research Agency)		Iringa
10. Mawasiliano na Uchukuzi	Zimamoto na Uokoaji	Hospitali ya Rufaa KCMC		Nkasi
11. Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto	Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa	Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma		Magu
12. Ofisi ya Waziri Mkuu				Bagamoyo
13. Kilimo na Chakula				Nzega
14. Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa				Shinyanga
15. Ujenzi				Kisarawe
16. Maliasili na Utalii				Tanga
17. Sayansi Teknolojia na Elimu ya Juu				Kyela
18. Mambo ya Ndani ya Nchi				Misungwi
19. Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa				Lindi DC
20. Elimu na Utamaduni				Mwanza
21. Mipango na Ubinafsishaji				Kilombero
22. Mambo ya Nje				Dodoma DC
23. Ardhi na Maendeleo ya Makazi				

Chanzo : Tume ya Utumishi wa Umma, 2005

4.2.3 Utayarishaji na Usambazaji wa Miongozo

Tume imetayarisha na kutoa miongozo kwa lengo la kuziwezesha Mamlaka mbali mbali za Ajira na Nidhamu pamoja na waajiri kutekeleza majukumu yao, Miongozo iliyotolewa ni:-

- Vitabu vya rejea 2,296 kuhusu sera, sheria, kanuni, taratibu za Utumishi wa Umma na nyaraka za Utumishi wa Umma.
- Miongozo 2,225 kuhusu masuala ya Ajira katika utumishi wa Umma, Toleo Na.1 mwaka 2004.
- Miongozo 1,800 kuhusu masuala ya Nidhamu na Rufaa katika Utumishi wa Umma, Toleo Na. 1 la 2005. ***Tazama Kiambatisho B.***

4.2.4 Ufuatiliaji wa Utayarishaji wa Taratibu za Uendeshaji (Service Schemes)

Kwa mujibu wa kifungu cha 7(2) cha Sheria Na.8 ya Utumishi wa Umma 2002, Waziri mwenye Dhamana ya Utumishi husika ndiye anayetakiwa kutayarisha Taratibu za Uendeshaji ambazo ni:-

- Taratibu za uendeshaji Serikalini
- Taratibu za uendeshaji Serikali za Mitaa
- Taratibu za uendeshaji Utumishi wa Walimu
- Taratibu za uendeshaji za Zimamoto, Uokoaji na Uhamiaji
- Taratibu za uendeshaji katika Utumishi wa Afya

Tume imekuwa ikihimiza Wizara zenye dhamana na Utumishi husika kwa mujibu wa kifungu cha 10 (1)(i) cha Sheria Na.8 ya Utumishi wa Umma 2002 kuhusu ukamilishwaji wa taratibu hizo ambapo hadi sasa bado hazijakamilika na kuanza kutumika. Taratibu hizo ziko kwenye hatua mbalimbali za ukamilishwaji.

4.2.5 Kupokea na Kushughulikia Rufaa.

Rufaa tano (5) zilishughulikiwa kwa mujibu wa kifungu cha 10 (1)(e) cha Sheria Na.8 ya Utumishi wa Umma 2002 na kutolewa uamuzi kama ifuatavyo:-

Jedwali la 9 : Rufaa Zilizowasilishwa Tume

Idadi ya Rufaa	Cheo	Mwajiri	Maamuzi
1	Mhasibu	Halmashauri ya Wilaya Mpanda	Rufaa yake ilikubaliwa. Alirudishwa kazini. Mashtaka yaanze upya kwa kufuata taratibu.
1	Mhasibu	Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo	Rufaa yake ilikubaliwa na alirudishwa kazini.
3	Afisa Ugavi	H/shauri ya Wilaya Bukoba	Rufaa zilirudishwa kupata uthibitisho kama taratibu zilifuatwa.
	Afisa Afya	H/shauri ya Wilaya ya Songea	"
	Daktari Msaidizi	Ofisi ya Katibu Tawala Tanga	"

Chanzo : Tume ya Utumishi wa Umma, 2005

5.0 UTEKELEZAJI WA MASUALA YA AJIRA NA NIDHAMU KATIKA UTUMISHI WA UMMA

Tume ilifanya ukaguzi na kutathmini hali ya Utumishi wa Umma kwa kuangalia vyombo vya umma vilivyopewa mamlaka ya usimamizi na uendeshaji wa Utumishi wa Umma kama vinatekeleza wajibu wao kulingana na sheria katika maeneo ya ajira, upandishwaji vyeo, mafunzo, nidhamu na rufaa.

5.1 Mbinu zilizotumika

Mbinu zilizotumika kujua hali ya utumishi kwa ujumla kwa misingi ya usimamizi na uendeshaji ni:

- Kufanya ukaguzi kwa mamlaka za ajira na nidhamu
- Kushiriki kwenye Kamati maalum za Ajira
- Kushiriki kwenye Bodi za Ajira
- Kufanya ziara Mikoani
- Kuchambua malalamiko yanayowasilishwa Tume.
- Kupitia taarifa mbali mbali zinazowasilishwa Tume kutoka Wizara na Taasisi mbalimbali za Umma.

Kwa kutumia mbinu hizo, Tume ilibaini mambo yafuatayo:-

5.2 Masuala ya Ajira

Mamlaka za Ajira zimeanza kutekeleza usimamizi na uendeshaji wa masuala ya ajira katika maeneo yafuatayo:-

5.2.1 Ajira na Uteuzi

Mamlaka za Ajira zimeanza kutekeleza ujazwaji wa nafasi wazi katika Utumishi wa Umma kwa kuzingatia misingi ya Sifa na ushindani ulio wazi kwa kupitia Kamati Maalum za Ajira, Bodi za Ajira, na Kamati za Mikoa na Wilaya. Ujazaji wa nafasi hizo unafanyika kwa njia ya Ajira mpya au kupandishwa vyeo watumishi waliomo kazini. Baadhi ya ajira zilizofanyika kwa njia ya ushindani na takwimu zake kupatikana kutokana na kushiriki kwa Tume kwa kipindi hiki, nafasi 3,585 zimejazwa kwa kufuata utaratibu mpya kama ifuatavyo:-

5.2.1.1. Kamati Maalum za Ajira

Kamati hizi ni za muda (Ad-hoc Committees) kwa mujibu wa Kanuni za utumishi wa Umma za 2003 Kanuni 9(3). Kamati zinaundwa na Wizara, Idara Zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa na Wakala wa Serikali pale ambapo pana shughuli ya kufanya inayohusu masuala ya Ajira, kupandisha vyeo na kuthibitisha kazini.

Katika kipindi hiki nafasi 2,950 zimejazwa na nafasi 801 hazikujazwa kama

inavyoonyeshwa kwenye mchanganuo hapa chini:-

Jedwali la 10 : Nafasi zilizojazwa kupitia Kamati Maalum za Ajira na uzingatiaji wa taratibu

1. WIZARA	Nafasi zilizojazwa	Nafasi ambazo hazikujazwa	Uzingatiaji wa taratibu	Ukiukwaji wa taratibu
Fedha	37			• Kuteua waombaji wenye sifa za chini kulinganishwa na walioachwa
Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo	68	1	√	
Viwanda na Biashara	21	3	√	
Ushirika na Masoko	16			• Kuitwa wasailiwa wasio na sifa
Maji na Maendeleo ya Mifugo	22	35	√	
Nishati na Madini	19	15	√	
Ofisi ya Makamu wa Rais	19	5		• Kamati kuundwa na wajumbe ambao sio watumishi wa ndani. • Kutangaza kazi ambayo haijapata kibali. • Wasailiwa wengi.
Mawasiliano na Uchukuzi	22	9		• Kuita waombaji wengi kwa siku moja.
Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto	49	13		• Kuteua waombaji kazi wengi kwa nafasi moja • Wasailiwa wengi kwa siku moja
Kilimo na Chakula	51	4	√	
* Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa	51	39	√	
Maliasili na Utalii	135	2		• Dalili za upendeleo kwa watumishi wa ndani kutokana na alama za wajumbe na namna msailiwa alivyojibu maswali. • Kurudia maswali kwa siku tofauti • Maandalizi hafifu ya

				makabrasha ya usaili

*** Watumishi wasio wanajeshi.**

Sheria na Mambo ya Katiba	38	2		• Kamati kujumuisha wajumbe wasio waajiriwa wa Wizara
* Mambo ya Ndani ya Nchi	162	32		• Matangazo yenye maelezo pungufu kama vile kazi atakayofanya atakapoajiriwa.
Elimu na Utamaduni	1475	332		• Kumteua mtumishi ambaye hakuomba kazi wala kuteuliwa.
Mambo ya Nje	20		√	
Ardhi na Maendeleo ya Makazi	50	11		• Dalili za upendeleo kwa watumishi wa Ndani ya Wizara
2. IDARA ZINAZOJITEMEGEA				
Tume ya Haki za Binadamu	50	96		• Sifa eg.G.P.A hazikuzingatiwa katika kuteua wasailiwa. • Dalili za upendeleo kwa watumishi wa ndani. • Wajumbe kutokuwa makini na kuheshimu kikao. Wametoka nje wakati msailiwa anajieleza. • Kurudia maswali kwa kada moja siku tofauti.
Tume ya Kudhibiti Madawa ya kulevya	2		√	
Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa	6			• Kutokuzingatia vigezo kama vile G.P.S wakati wa kuteua wasailiwa. • Dalili za upendeleo. • Kutokuwepo kwa maswali maalum (structured questions)
Idara ya Mahakama ya Rufaa	96	105		• Kuitwa wasailiwa ambao hawakutuma maombi ya kazi. • Kuitwa wasailiwa wengi sana kwa siku moja. • Kuita wasailiwa wasio

				na sifa. • Dalili za upendeleo.

*** Watumishi wasio Askari**

Tume ya Kurekebisha Sheria	3		√	
Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali	53			• Maswali yasiyohusiana na maudhui ya usaili
Tume ya Taifa ya Uchaguzi	7	7	√	
Uhamiaji	270		√	
Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi	23	2	√	
Tume ya Utumishi wa Umma	34	82	√	
3. Wakala wa Serikali				
Wakala wa Ndege za Serikali	12		√	
4. Sekretarieti za Mikoa				
Tanga	21	2	√	
Mtwara	19		√	
Singida	7	1	√	
Mara		3	√	
Iringa	60		√	
Arusha	32		√	
JUMLA	**2950**	**801**	√	

Chanzo : Tume ya Utumishi wa Umma, 2005



Chanzo : Tume ya Utumishi wa Umma, 2005

Takwimu hizi zinaonyesha kwamba bado kuna ukiukwaji taratibu katika kushughulikia masuala ya ujazaji wa nafasi wazi katika utumishi wa umma.

5.2.1.2 Bodi za Ajira

Bodi hizi zinaundwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kama ilivyoanishwa na Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003, Kanuni 127. Majukumu ya Bodi hizi ni kushughulika na mchakato wa masuala ya Ajira kama vile kufanya usaili kwa ajira mpya, kuwapandisha vyeo na kuthibitisha watumishi na kuwasilisha matokeo kwa Mamlaka ya Serikali ya Mtaa husika.

Katika kipindi hiki Bodi za Ajira 114 zimeundwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Nafasi 423 zimejazwa na Halmashauri 22 ambapo nafasi 191 hazikujazwa. Aidha

Halmashauri 2 zilikiuka taratibu kama inavyoonyesha kwenye jedwali hapa chini.

Jedwali la 11 : Nafasi zilizojazwa kupitia Bodi za Ajira

Bodi za Ajira (Halmashauri)	Nafasi Zilizojazwa	Nafasi ambazo hazikujazwa		
		Kukosa sifa	Kutofika kwenye usaili	Kutofuata taratibu
Kondoa	8	14	-	-
Kibaha	17		-	-
Rombo	18	2	-	-
Arusha	2	1	-	-
Ngorongoro	16	12	-	-
Serengeti	26	-	27	-
Same	13	4	-	-
Iringa	20	34	-	-
Nkasi	10	-	10	-
Magu	13	16	-	-
Bagamoyo	26	5	1	-
Misungwi	19	3	-	-
Lindi DC	10		10	-
Mwanza	44		-	-
Kilombero	8	6	-	-
Dodoma DC	8	-	-	-
Nzega	22	-	16	1
Shinyanga	3	-	3	
Kisarawe	73	-	18	-
Tanga	44	-	4	-
Kyela	23	-	5	-
Mbulu	-	-	-	1
JUMLA	423	97	94	2

Chanzo : Tume ya Utumishi wa Umma, 2005



Chanzo : Tume ya Utumishi wa Umma, 2005

Takwimu hizi zinaonyesha kwamba kuna uzingatiwaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu za ajira kwa kiwango kikubwa katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa zilizofanya ajira.

5.2.1.3 Kamati za Mikoa na Wilaya

Kamati hizi zimeundwa na Tume ya Utumishi wa Umma kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma 2003, Kanuni 113, 114 na 120 na jukumu la Kamati hizi kushughulika na mchakato wa masuala ya Ajira kwa Walimu kama vile Ajira mpya, usajili wa walimu, kupandisha vyeo na kuthibitisha kazini na kusimamia maadili ya walimu. Katika kipindi hiki Kamati za Ajira za Mikoa 21 na Wilaya 113 zimeundwa, hivyo kwa ujumla zipo 134. Kamati za Wilaya 27 zimejaza

nafasi 212 za Walimu na nafasi 19 hazikujazwa kama inavyoonyeshwa hapa chini.

Jedwali Na.12: Nafasi zilizojazwa kupitiaKamati za Wilaya

NA.			NAFASI HAZIKUJAZWA	
	KAMATI ZA WILAYA	NAFASI	KUKOSA SIFA	KUTOFIKA
1.	MKURANGA	1		
2.	RUJEWA	19		
3.	SUMBAWANGA	8		
4.	MAKETE	4		
5.	DODOMA	11	1	
6.	KONGWA	11		
7.	MBINGA	9		
8.	DODOMA MANISPAA	9		
9.	MPWAPWA	5		
10.	KOROGWE	4		
11.	ILALA	14		
12.	GEITA	7		
13.	SIMANJIRO	2		
14.	TANDAHIMBA	5		
15.	MTWARA	2		
16.	BAGAMOYO	21	4	
17.	KIBAHA	2		
18.	BABATI	7	1	
19.	MONDULI	16		
20.	BUNDA	17		
21.	SONGEA	2		
22.	NZEGA	-1	1	
23.	TABORA (V)	4		
24.	KISARAWE	3	-	1
25.	SHINYANGA MANISPAA	2	10	
26.	HANDENI	5	1	
27.	TARIME	23		
	JUMLA	**212**	**18**	**1**

** Jedwali linaonyesha kuwa taratibu za Ajira zilifuatwa*

Jedwali 13: Nafasi Ambazo Hazikujazwa

Kamati/Bodi	Nafasi zilizojazwa	Nafasi zilizokosa watu wenye sifa	Hawakufika kwenye usaili
Kamati Maalum za Ajira	2,950	801	0
Bodi za Ajira	423	97	94

Kamati za Wilaya	212	18	0
Jumla	3,585	916	94

Chanzo: Tume ya Utumishi wa Umma, 2005



Chanzo: Tume ya Utumishi wa Umma, 2005

Chati hii inaonyesha kwamba Kamati Maalum za Ajira zinaongoza kwa kuwa na nafasi zilizokosa watu wenye sifa zikifuatwa na Bodi za Ajira na mwisho Kamati za Wilaya.

Pamoja na sababu zilizotajwa za kutokujaza nafasi wazi zipo sababu nyingine kama vile mwajiri kutokuomba kibali au kutotangaza nafasi wazi. Tume haikuweza kufuatilia na kupata takwimu za nafasi wazi zilizokuwepo ambazo hazikujazwa katika mwaka huu wa fedha. Kazi hii itafanywa katika mwaka wa fedha ujao.

5.2.2 Upungufu uliojitokeza.

Katika mchakato wa ujazaji wa nafasi zilizo wazi kwa kutumia Kamati Maalum za Ajira na Bodi za ajira Tume iligundua ukiukwaji wa taratibu za ajira kama ifuatavyo:-

- Kuitwa kwenye usaili watu wasio na sifa. Hali hii imejitokeza katika Halmashauri ya Wilaya Mbulu kwa kufanya usaili wa Madereva wa darasa la VII badala ya wenye sifa ya chini ya Kidato cha Nne.
- Kusaili watu ambao hawajaomba nafasi hizo. Hili limejitokeza katika Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi na Idara ya Mahakama kwa nafasi za Madereva na Katibu Muhtasi.
- Kuteuliwa mtu ambaye hakuomba cheo wala hajafanya usaili. Hili lilionekana katika Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa nafasi ya Mkurugenzi Msaidizi.
- Kutokuwepo na maswali maalumu ya usaili, hivyo kupelekea kutokuwepo na usawa katika kutoa alama kwa wasailiwa. Hili limejitokeza katika Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kwa nafasi za Wakili wa Serikali, Udereva na Afisa Tawala.
- Kutumia kura badala ya kutoa alama kwa kuzingatia matokeo ya usaili. Hili lilifanyika Halmashauri ya Wilaya ya Nzega.

5.2.3 Upandishwaji Vyeo.

Baadhi ya Watumishi waliokuwepo kwenye Utumishi wa Umma wamepanda vyeo kwa njia ya ushindani ulio wazi baada ya kuomba nafasi za juu zilizotangazwa, nje au ndani na mwajiri wake. Kwa mfano watumishi 59

wamepanda vyeo na kuchukua nafasi za Katibu Tawala Wasaidizi wa Mikoa.

5.2.4 Kuthibitishwa kazini

Katika kipindi hiki kamati Maalum ya Ajira imeweza kufanya mchakato wa kumwezesha Katibu Tawala wa mkoa wa Mwanza kuwathibitisha watumishi 20 na Dodoma watumishi 43. Tume haikuweza kupata taarifa za uthibitishwaji kazini kutoka kwa Mamlaka nyingine za Ajira.

5.2.5 Maendeleo ya Watumishi

Waajiri wanawajibu wa kuangalia maendeleo ya watumishi wao na kuona kwamba yanaendana na matakwa yanayotakiwa kwa kila mtumishi kulingana na kazi anayofanya. Mpaka sasa kuna jumla ya watumishi 110,636 ambao hawana Elimu ya Kidato cha Nne. Serikali imetoa muda hadi mwaka 2007 watumishi hao wawe wamejiendeleza. Kuna baadhi ya sekta ambazo zitaathirika zaidi na sera hii kama vile sekta za Afya na Zimamoto na Uokoaji. Hata hivyo takwimu sahihi kwa upande wa Sekta ya Afya hazijakusanywa, bali kwa upande wa sekta ya Zimamoto kati ya watumishi 619 watumishi wa darasa la VII ni 480 sawa na asilimia 77.45. Huu ni mfano kwa baadhi ya sekta, Idara/Wizara ambazo zitaathirika endapo watumishi hawa hawatatimiza sifa hizo ifikapo mwaka 2007. Pamoja na nia nzuri ya Serikali kuendeleza watumishi wake si busara kwa Serikali kuwaachisha kazi baada ya mwaka 2007. Athari zake zinaweza kuwa kubwa kwa Serikali kubadilisha Muundo

wa Utumishi wao. Tume inapendekeza kuwa kwa wale watakaoshindwa kufikia kiwango cha sekondari, waendelee kufanya kazi hadi watakapoondoka wenyewe kwa sababu ya utumishi wao kukoma kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo. Na kwa upande wa Utumishi maalumu wa Zimamoto, jitihada zifanyike kwa kuangalia uwezekano wa kuusaidia katika athari zitakazojitokeza kutokana na viwango vya chini ya elimu vilivyoonyeshwa.

5.3 Masuala ya nidhamu

Katika kipindi hiki Mamlaka za Nidhamu zimeanza kutekeleza uendeshaji wa masuala ya nidhamu kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Uendeshaji katika Utumishi wa Umma na mwongozo wa Tume kuhusu masuala ya nidhamu na rufaa.

Utafiti wa awali uliofanywa na Tume kwa kuangalia
baadhi ya mashauri yaliyowasilishwa umebaini kuwa watumishi wa umma wanatofautiana kisekta katika aina ya makosa kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapa chini :

Jedwali 14 : Aina ya Makosa

MAKOSA	Waalimu	Serikali za Mitaa	Serikalini
Kughushi	22	-	-
Kukaririsha	3	-	-
Kutotii mamlaka	17	2	2
Kutowajibika/uzembe	23	3	2
Kutishia kuua	2	-	-
Lugha chafu	40	-	-
Mapenzi na wanafunzi	52	-	-
Ugomvi	4	-	-
Ulevi	46	-	-
Utapeli/wizi	19	-	1
Utoro	252	-	10
Kubaka/kulawiti	2	-	-
Kuchochea migomo	2	-	-
Kudhalilisha	5	-	-

Ualimu hewa	3	-	-
Ubadhirifu		7	5
Upotevu hati		-	2
Udanganyifu		-	1
Jumla	492	12	23

Chanzo : Tume ya Utumishi wa Umma, 2005

Chati 7 : Asilimia ya Mashauri Yaliyoripotiwa na Utumishi wa Waalimu



Chanzo : Tume ya Utumishi wa Umma, 2005



Chanzo : Tume ya Utumishi wa Umma, 2005



Chanzo : Tume ya Utumishi wa Umma, 2005

Hali hii inaonyesha kuwa utoro kazini ndilo kosa linalojitokeza zaidi miongoni mwa Walimu kwa asilimia 52 ya makosa yote, na Utumishi Serikalini ni asilimia 43. Hii inaonyesha kwamba watumishi wa umma wanakwenda sehemu nyingine kwa ajili ya

maslahi bora zaidi au wanajishughulisha na shughuli nyingine wakati wa saa za kazi. Katika Utumishi wa Serikali za Mitaa asilimia 58 ya makosa imetokana na ubadhirifu. Hii inaonyesha kwamba kuna haja ya kuimarisha usimamizi na udhibiti wa mali ya umma kwenye sekta hii.

5.3.1 Mashauri yalivyoshughulikiwa na Mamlaka za Nidhamu

Kwa sababu ya upungufu wa watumishi, Tume haikuweza kufanya ukaguzi wa kina kwa mashauri yote yaliyoshughulikiwa na Mamlaka za Nidhamu, kwa mujibu wa Sheria Na.8 ya mwaka 2002 na Kanuni zake. Mashauri 448 yaliyowasilishwa na kushughulikiwa na Tume yameonyesha kuwa Mamlaka za Nidhamu hazikuzingatia taratibu na kanuni katika kushughulikia masuala ya nidhamu kama inavyoonyesha katika mchanganuo ufuatao:-

- **Mashauri yaliyowasilishwa ya Tume zilizovunjwa**

  Katika Mashauri 443 yaliyowasilishwa, kuna Mashauri 73 yanayoonyesha kuwa Mamlaka za Nidhamu zilikiuka taratibu za kuwachukulia hatua watumishi kama inavyoonyeshwa hapa chini:

Jedwali 15 :Ukiukwaji wa taratibu Katika Kuendesha Mashauri ya Nidhamu ya Tume zilizovunjwa

Tume za Utumishi zilizovunjwa	Taratibu kufuatwa	Taratibu kutofuatwa	Jumla
Utumishi Serikalini	16	12	28
Utumishi wa Serikali za Mitaa	4	8	12
Utumishi wa Ualimu	350	53	403
Jumla	370	73	443

Chanzo : Tume ya Utumishi wa Umma



Chanzo : Tume ya Utumishi wa Umma, 2005

Hii inaonyesha kwamba mashauri mengi yaliyochukuliwa dhidi ya watumishi Serikali za Mitaa kulikuwa na ukiukwaji zaidi ikifuatiwa na Utumishi Serikalini.

- **Mashauri yaliyoshughulikiwa na Tume kwa mujibu wa Sheria Na. 8 ya mwaka 2002.**

  Katika kipindi hiki mashauri matano ya rufaa yaliwasilishwa Tume. Rufaa zote tano zilionyesha kuwa kulikuwa na ukiukwaji wa taratibu. Katika kuwachukulia watumishi hatua za Nidhamu kati ya mashauri hayo Rufaa mbili zilikubaliwa kutokana na ukiukaji wa taratibu wakati rufaa tatu uamuzi haukutolewa kwa kuwa hazikufuata utaratibu.

Jedwali 16 : Ukiukwaji wa taratibu Katika Kuchukua Hatua za Nidhamu kwa mujibu wa Sheria Na.8 ya mwaka 2002

Utumishi	Taratibu kufuatwa	Taratibu kutofuatwa	Jumla
Utumishi Serikalini	0	1	1
Utumishi wa Serikali za Mitaa	0	4	4
Jumla	0	5	5

Chanzo : Tume ya Utumishi wa Umma, 2005

5.3.2 Upungufu uliojitokeza katika kushughulikia masuala ya nidhamu

Baadhi ya Mamlaka za Nidhamu zimeonyesha upungufu ufuatao:-

- Mamlaka za Nidhamu kutofuata kanuni ambazo zinaitaka mamlaka husika kuanzisha mashtaka ya nidhamu na kusaini hati za mashtaka na barua za adhabu.
- Mamlaka ya Nidhamu kutowapatia nafasi ya kujitetea watumishi waliokuwa wakikabiliwa na mashauri ya Nidhamu.
- Baadhi ya Mamlaka za Nidhamu kuwafungulia mashitaka ya nidhamu kwa makosa yale yale ambayo mahakama iliwaachia huru ambapo ni kinyume cha sheria.
- Kukosekana kwa hati za mashitaka wakati wa uanzishaji wa mashitaka ya nidhamu au kutoteuliwa kwa Kamati Maalum za Uchunguzi.
- Hati za mashtaka kutokuonyesha bayana kosa lililotendwa na Mtumishi.

6.0 ZIARA ZA TUME

Pamoja na kuanzishwa kwa Mfumo wa Uboreshaji Utendaji kazi Serikalini kwa kuzingatia Sheria Na.8 ya Utumishi wa

Umma, bado kuna maeneo ambayo yanahitaji kuboreshwa zaidi katika utekelezaji wake. Hii imedhihirika kwenye Ziara zilizofanywa na Tume Mikoani katika kipindi hiki. Baadhi ya maeneo ambayo yanahitaji kuboreshwa katika utekelezaji wake ni:-

6.1 Upandishwaji Vyeo:

Baadhi ya Watumishi hawajapandishwa vyeo kwa muda mrefu, hivyo hawajui hatima yao baada ya kuanzishwa mfumo mpya ambapo nafasi zote za vyeo mbalimbali zinashindaniwa. Suala hili lilijitokeza wakati wa Ziara za Tume. Aidha, Tume imepokea barua 219 za malalamiko kutoka kwa watumishi.

6.2 Utekelezaji wa Miundo Mipya ya Utumishi.

Katika utekelezaji wa miundo mipya ilionekana kuwa baadhi ya watumishi wamelundikwa kwenye ngazi moja pamoja na walioajiriwa hivi karibuni. Hali hii iliwakatisha tamaa watumishi walioanza kazi muda mrefu na hivyo kupunguza tija na ari ya kazi. Hata hivyo suala hili limechukuliwa hatua na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa kuwataka waajiri waorodheshe watumishi husika na zoezi hilo na kuambatanisha makisio ya gharama za kuwapandisha vyeo walivyokuwa wanastahili ili tatizo hili lishughulikiwe.

6.3 Uhamisho,

Suala la uhamisho nalo lilijitokeza kwa watumishi ambao wamekaa kituo kimoja kwa muda mrefu. Watumishi hao walijulishwa kuhusu utaratibu wa uhamisho kuwa utafanywa na Katibu Mkuu Ofisi ya

Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na kwamba utafanywa ikiwa ni kwa manufaa ya Umma. Uhamisho unaohusika na utaratibu huu ni ule wa kutoka Wizara, Idara au Mamlaka za Serikali za Mitaa moja kwenda nyingine.

6.4 Mafunzo kwa Watumishi

Ilionekana kuwa baadhi ya waajiri wanashindwa kuwaendeleza watumishi wao kwa kuwapatia mafunzo na ujuzi kutokana na kwamba hawana Mipango ya mafunzo, hivyo hawatengi fedha za kutosha kwa ajili ya mafunzo kwenye bajeti zao. Aidha, fedha zinazotengwa katika bajeti ni kidogo. Tume iliwaelekeza waajiri hao kuhusu umuhimu wa kuwaendeleza watumishi wao kwa kuandaa Mpango wa Mafunzo unaotengewa fedha kila mwaka.

6.5 Utaratibu wa OPRAS

Imebainika kuwa utaratibu huu haujaeleweka vizuri kwa Waajiri pamoja na watumishi wenyewe kuhusu namna ya kuutekeleza, faida zake na uwekaji malengo yenye kupimika. Suala hili linafanyiwa kazi na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa kutoa mafunzo kwa Waajiri na Watumishi katika Utumishi wa Umma.

6.6 Mfuko wa Bima ya Afya.

Watumishi wa Umma wamedai kuwa mfuko huo hauwahudumii kikamilifu na hivyo kutonufaika na michango yao. Aidha, watumishi wangependa mfuko uhudumie magonjwa yote na kuwapatia dawa. Suala hili limefikishwa kwa mamlaka husika ya Mfuko huo. Aidha,

Mfuko wa Bima ya Afya umeanza kushughulikia suala hili kwa kutoa madodoso ili kupata maoni ya wadau kuhusu huduma unazotoa.

6.7 Malipo yanayoendana na Stahili zao za kazi

Baadhi ya watumishi wamedai kuwepo kwa ucheleweshaji au kutokulipwa stahili zao kama vile; malipo ya hitimisho la kazi, Malipo ya posho mbalimbali, nauli za likizo, kurekebishiwa mishahara, na mapunjo ya mishahara. Suala hili limefikishwa kwa wahusika ambao ni Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na HAZINA.

6.8 Mishahara na stahili mbalimbali za Watumishi

Tatizo la maslahi na mishahara ya watumishi wa Umma kutofautiana sana miongoni mwao nalo lilijitokeza na kutolewa mfano wa Watumishi wanaofanya kazi Mamlaka ya Mapato Tanzania na Wakala wa Serikali kuwa na mishahara mikubwa ikilinganishwa na ile ya watumishi wanaofanya kazi katika Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.Ili watumishi wa Umma wa Tanzania wafanye kazi kwa ufanisi kwa lengo la kuwa na Utumishi uliotukuka iko haja ya kuoanisha maslahi yote na hasa mishahara.

6.9 Masuala ya Mirathi

Katika ziara hizo suala la kucheleweshwa malipo ya mirathi pia lilijitokeza kwamba inachukua muda mrefu kwa sababu mbalimbali zikiwemo za urasimu na kutokamilisha hati muhimu kwa wahusika wa mirathi. Ipo haja ya kuboresha taratibu za kukamilisha ulipaji wa

malipo hayo na kuwaelimisha watumishi kuhusu taratibu za mirathi zinazotakiwa.

7.0 BARUA ZA MALALAMIKO ZILIZOPOKELEWA TUME

Barua 27,741 zilizopokelewa Tume katika kipindi hiki zenye malalamiko mbalimbali kama ilivyoonyeshwa kwenye Jedwali hapa chini.

Jedwali 17 : Malalamiko ya Watumishi

Malalamiko ya watumishi wa umma kisekta	Afya	Ualimu	Serikali za Mitaa (Kilimo)	Zimamoto na Uokoaji	Utumishi serikalini	Jumla
Kutopandishwa cheo	87	0	102	20	10	219
Kutobadilishwa vyeo baada ya kupata sifa	5	0	0	1	0	6
Malalamiko kutokulipwa baada ya kuhamishwa	2	7,559	0	0	0	7,561
Kutorekebishiwa/kutolipwa mishahara	6	12,235	0	2	1	12,244
Madai ya kulipwa fedha ya likizo	6	7,586	0	0	0	7,592
Kupunguzwa kazini	1	0	0	0	0	1
Kustaafishwa kwa manufaa ya umma	1	0	0	0	0	1
Unyanyasaji kazini	1	0	0	4	0	5
Kufutwa kwenye Payroll	0	112	0	0	0	112
Jumla	109	27,492	102	27	11	27,741

Chanzo : Tume ya Utumishi wa Umma, 2005



Chanzo : Tume ya Utumishi wa Umma, 2005

Katika kukamilisha kazi za Tume zilizovunjwa jumla ya walimu 30,434 walipandishwa vyeo na 1,335 walibadilishwa vyeo ndio maana malalamiko yao yanahusu kutorekebishiwa stahili zao mbalimbali wakati kada zingine Kilimo, Afya na Zimamoto na Uhamiaji madai yao ni kutopandishwa vyeo.

Baadhi ya malalamiko yaliyopokelewa yameshughulikiwa na Tume.Aidha,kwa wale ambao hawajashughulikiwa wameelekezwa kwamba masuala yao yatashughulikiwa na Waajiri wao kwa mujibu wa Sheria Na.8 ya mwaka 2002, Kanuni na Taratibu za Uendeshaji za mwaka 2003 na Waraka wa Utumishi Na.1 wa mwaka 2004.

8.0 HATUA ZILIZOCHUKULIWA NA TUME KUKABILIANA NA KASORO ZILIZOJITOKEZA

Kutokana na Upungufu uliojitokeza kama ilivyoelezwa kwenye ibara 5.2.2 na ibara 5.3.2. Tume ilibaini kuwa upungufu huo umetokana ama na utata uliopo katika Sheria au Mamlaka husika kutofahamu vizuri Sheria, Kanuni na Taratibu za Uendeshaji wa Utumishi wa Umma. Tume ilichukua hatua zifuatazo:

- Kuainisha maeneo yenye utata na migongano katika utekelezaji wa Sheria Namba 8 ya Mwaka 2002 na Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 na Taratibu za Uendeshaji za Mwaka 2003, na kuyapeleka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili sheria iweze kurekebishwa.
- Kubatilisha matokeo ya usaili pale ambapo taratibu zilikiukwa na kuagiza zoezi hilo lifanyike upya kwa kufuata taratibu. Kwa mfano katika Halmashauri ya Wilaya Mbulu na Nzega. Aidha, Tume inaendelea na uchunguzi kuhusu ukiukwaji wa taratibu za ajira uliofanyika katika Wizara ya Elimu na Utamaduni kuhusu ajira ya Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu ya Msingi.
- Kutoa mafunzo na kusambaza miongozo kwa Mamlaka za Ajira na Nidhamu pamoja na Waajiri ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kwa urahisi kwa mujibu wa sheria.
- Kutoa maelekezo kwa njia ya waraka kuhusu uzingatiaji wa Sheria na Kanuni katika kushughulikia mashauri ya Ajira na Nidhamu, hasa mkazo umesisitizwa kwa

Mamlaka ya Nidhamu kwamba ndizo zinapaswa kuanzisha mashtaka na kutoa adhabu.

- Kuuandikia Mfuko wa Bima ya Afya kushughulikia, kuboresha na kuyapatia ufumbuzi masuala yaliyolalamikiwa kuhusiana na huduma zinazotolewa na mfuko huo.

9.0 HALI YA FEDHA

Katika kipindi cha Julai 2004 hadi Juni 2005, Tume ilitengewa fedha kiasi cha Tshs. **6,669,097,900/=** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake na mgawanyo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:-

- Mishahara ya watumishi (Personal Emoluments). Tshs. **1,929,190,900/=**
- Utoaji huduma kwa wadau (Service Delivery), Tshs. **3,296,893,100/=**
- *Maendeleo ya watumishi (Capacity Building) na Tshs **1,040,330,900/=**
- Kuboresha ofisi na kununua vitendea kazi (Capital Investment) Tshs. **402,683,000/=**

**** Tazama Kiambatisho C***

10.0 CHANGAMOTO KWA TUME YA UTUMISHI WA UMMA

Kazi kubwa ya Tume ni kuhakikisha kuwa masuala yote ya utumishi yanaendeshwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za uendeshaji katika utumishi wa umma, kwa mfano Ajira inazingatia sifa, uwezo na ushindani na masuala ya nidhamu yanaendeshwa kwa misingi ya haki na usawa.

Kutokana na dhana hiyo, changamoto kubwa kwa Tume ni hizi zifuatavyo;

- Kufanya shughuli za Tume ambazo kwa kipindi hiki hazikuweza kufanyika kama vile kufuatilia na kutathmini utendaji kazi wa watumishi wa Umma wa ngazi mbalimbali ili uwe na ufanisi unaojali wateja na wenye kuzingatia matokeo.
- Kuwa na Rasilimali watu wa kutosha na wenye ujuzi. Hii ni pamoja na vitendea kazi kama vile kompyuta, magari na samani za ofisi kwa ajili ya kufanya ukaguzi na tathmini.
- Kuhakikisha kwamba watumishi wa Tume wanapatiwa mafunzo ya kutosha ili kuweza kumudu majukumu yao.
- Kuziwezesha Mamlaka za Nidhamu na Ajira pamoja na watumishi kwa kuzipatia maelekezo na kutoa miongozo itakayowasaidia kuwa na tafsiri sahihi na inayofanana katika utekelezaji wa majukumu yao.
- Kuhakikisha kuwa Mamlaka za Ajira na Nidhamu zinatekeleza majukumu yao kwa kufuata Sheria, Haki, Usawa na Uwazi.
- Kuhakikisha kuwa Taratibu za Uendeshaji (Service Schemes) zilizotajwa kwenye sheria ya utumishi wa umma zinakamilika na kuanza kutumiwa na mamlaka za Ajira na Nidhamu pamoja na Waajiri.
- Kuwahimiza waajiri kuhakikisha kuwa watumishi waliopo kwenye utumishi ni wale wenye sifa zinazotakiwa kwa mujibu wa sera, sheria na miundo ya utumishi.
- Kuhakikisha kuwa Watendaji Wakuu katika usimamizi wa nidhamu wanawajibika na usimamizi thabiti wa Utumishi wa Umma kwa madhumuni ya kuleta ufanisi na tija.
- Kuhakikisha kuwa watumishi na Watendaji Wakuu katika Utumishi wa Umma wanabadilika kimtazamo katika utendaji kazi ili kuendana na matakwa ya sheria katika Utumishi wa Umma.

- Kufuatilia na kuona kwamba kila mwajiri anaweka kumbukumbu za watumishi vizuri na Tume itazikusanya, kuzihakiki na kuzihifadhi kwa ajili ya shughuli za Tume.

11.0 MATARAJIO YA TUME YA UTUMISHI WA UMMA.

Katika kipindi kijacho, Tume ya Utumishi wa Umma inatarajia kufanya mambo yafuatayo:-

- Kufanya ukaguzi wa kina katika Wizara, Idara zinazojitegemea,Wakala za serikali na kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kutumia mwongozo wa ukaguzi (Human Resource Audit Manual) utakaotolewa na Tume.
- Kuwawezesha watumishi wake (capacity building) ili kuweza kumudu vema majukumu yao.
- Kwamba Taratibu za Utumishi (service scheme) ziwe zimekamilika na kuanza kutumika.
- kuhakikisha Mfumo wa Uboreshaji wa Utendaji Kazi Serikalini unakamilika katika Wizara, Idara zinazojitegemea,Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi zote za Serikali ili kuleta tija,uwajibikaji na uboreshaji wa utoaji huduma.
- Kuwa Mamlaka za Ajira na Nidhamu zinatekeleza majukumu yao kulingana na matakwa ya sheria, kanuni na taratibu za uendeshaji za utumishi wa umma.
- Kuhakikisha kuwa watumishi watafanya kazi zao kwa kuzingatia maadili ya utumishi wa umma.
- Kupata ushirikiano toka kwa Mamlaka za Ajira na Nidhamu pamoja na watumishi wa Umma katika kuboresha Utumishi wa Umma.
- Kutekeleza majukumu yake kwa wakati, uwazi na kwa misingi ya haki na usawa kwa wadau wake wote.

12.0 HITIMISHO

Tume ya Utumishi wa Umma imejizatiti kutoa huduma kwa watumishi wa Umma na Mamlaka za Ajira na Nidhamu kwa misingi ya haki, usawa na uwazi kwa kuzingatia Sera ya Ajira na Menejimenti ya Utumishi wa Umma 1998, Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya 2002 na Kanuni na Taratibu zake za mwaka 2003. Ni matumaini ya Tume kwamba, watumishi na mamlaka hizo watatekeleza wajibu wao kwa misingi ya sheria katika utoaji huduma bora kwa wananchi kwa ufanisi na kwa viwango vya juu ili kuleta maendeleo ya nchi yanayoendeleza hali ya maisha, kuondoa umasikini na kuongeza ustawi wa jamii hivyo kuufanya Utumishi wa Umma kuwa uliotukuka.

INAWASILISHWA NA

JINA	**SAINI**
1. Jaji Mstaafu Lameck M. S. Mfalila	……
2. Bw. Leonard K. Msaki	……
3. Bibi Monica G. Mbapila	…… …
4. Balozi Norman A. Kiondo	……..
5. Bibi Nderikyo E. Ligate	…… ……. …..
6. Bw. Ashour A. Abbas	…… ……
7. Bw. Kenya A. Hassan	……
8. Bibi Thecla W. Shangali	…….. . ……